# HALMASHAURI YA WILAYA YA HANDENI

## MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI CHA TAREHE 05/07/2021

**WALIOHUDHURIA**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. Bw. Napoleon Mlowe | - | DLNRO | - | Mwenyekiti |
| 2. Bw. Brian M. Munga | - | HPMU | - | Katibu |
| 3. Bi. Edina A. Katalaiya | - | DPLO | - | Mjumbe |
| 4. Bw. Sekiara Kiariro | - | DLFO | - | Mjumbe |
| 5. Mwl. Gosbert Damazo | - | DSEO | - | Mjumbe |

**AMBAO HAWAJAHUDHURIA**

1. Dr. Ipyana F. Mwandelile - DMO - Amehamishwa kituo cha kazi

**SEKRETARIET**

1. Bw. Selemani Mhunga

**MUHTASARI NA. 01/2021/2022:- KUFUNGUA KIKAO**

Katibu aliwafahamisha wajumbe kuwa kikao hicho ni kikao cha Kawaida, na kumkaribisha Mwenyekiti afungue kikao na Mwenyekiti alifungua kikao saa 06.17 mchana.

**MUHTASARI NA. 02/2021/2022:- KUTHIBITISHA AGENDA.**

Katibu aliwasilisha agenda zitakazojadiliwa kama ifuatavyo:-

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha agenda
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha Bodi ya Zabuni kilichofanyika tarehe 12/04/2021
4. Kupitia taarifa ya manunuzi kipindi cha robo ya nne ya mwaka wa fedha 2020/2021.
5. Kupitia taarifa ya manunuzi kwa njia ya circular Resolution
6. Kupitia taarifa ya manunuzi ya jengo la ofisi ya Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2020/2021.
7. Kupitia taarifa ya manunuzi ya Hospitali ya Wilaya kwa mwaka wa fedha 2020/2021
8. Kuomba kibali cha kutekeleza miradi ya maendelezo kwa njia ya nguvu kazi (Force Account).
9. Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti
10. Kufunga kikao.

Wajumbe walipitia agenda zilizowasilishwa na kuridhia zijadiliwe.

**MUHTASARI NA. 03/2021/2022:- KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA TAREHE 12/04/2021.**

Muhtasari wa kikao cha Bodi ya Zabuni kilichofanyika tarehe 12/04/2021 ulisomwa na wajumbe kuupokea na kuthibitishwa kwa ajili ya kumbukumbu za Halmashauri.

**MUHTASARI NA. 04/2021/2022:- KUPITIA TAARIFA YA MANUNUZI KIPINDI CHA ROBO YA NNE YA MWAKA WA FEDHA 2020/2021.**

Katibu wa Bodi (Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi) aliwasilisha taarifa ya manunuzi ya Halmashauri yaliyofanyika katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka wa fedha 2020/2021.

Akiwasilisha aliwaeleza wajumbe kuwa katika kipindi cha mwezi Aprili hadi Juni 2021 Halmashauri ya Wilaya ya Handeni ilifanya manunuzi yenye jumla ya shilingi 1,134,270,771. Manunuzi hayo yalifanyika kwa njia ya Hati agizo (LPO).

Bodi ilijadili taarifa manunuzi ya Halmashauri yaliyofanyika katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka wa fedha 2020/2021 na kuipitisha kwa kushauri yafuatayo:-

i. Taarifa ya mchanganuo wa manunuzi ioneshe aina ya kifaa kilichonunuliwa au huduma iliyotolea pamoja na gharama zake.
ii. Taarifa ya manunuzi yaliyofanyika katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2020/2021, Idara ya Elimu ~~msingi na~~ sekondari hazikuonekana na haikuwasilishwa hivyo Bodi iliagiza wakati wa kuandaa michanganuo ya taarifa za manunuzi ufuatiliaji wa karibu ufanyike na taarifa zioneshwe Ki-idara. Aidha taarifa ya manunuzi ya Idara za Idara za Msingi na Sekondari ziwasilishwe kikao kijacho.

**MUHTASARI NA. 05/2021/2022:- KUPITIA TAARIFA YA MANUNUZI KWA NJIA YA CIRCULAR RESOLUTION.**

Katibu wa Bodi aliwasilisha taarifa ya manunuzi yaliyofanyika kwa njia ya Circular Resolution na wajumbe kuipokea.

Akiwasilisha aliwaeleza wajumbe kuwa katika kipindi cha robo ya nne Kitengo kimesimamia manunuzi ya mafuta kwa ajili ya uendeshaji wa ofisi na vitendea kazi vya ofisi kama ifuatavyo:-

| NA. | AINA YA MANUNUZI | KIASI |
|---|---|---|
| 1 | Manunuzi ya mafuta kwa Idara ya fedha | 4,089,994.23 |
| 2 | Manunuzi ya mafuta Idara ya Mipango | 3,878,000 |
| 3 | Manunuzi ya mafuta kiwanda cha matofali | 4,438,000 |
| 4 | Manunuzi ya mafuta Idara ya Ujenzi | 4,438,000 |
| 5 | Manunuzi ya mafuta Idara ya Utawala | 4,438,000 |
| 6 | Manunuzi ya mafuta shughuli za mwenge wa Uhuru 2021 | 5,214,650 |
| 7 | Manunuzi ya kompyuta, fotokopi, scanar na Printer kwa matumizi ya ofisi (Elimu msingi) | 163,350,000 |
| 8 | Manunuzi ya wino na fotokopi mashine pamoja na Printer | 13,750,000 |
| 9 | Manunuzi ya rimu za karatasi kwa ajili ya matumizi ya ofisi | 20,600,000 |
| | **JUMLA** | **224,196,644.23** |

Wajumbe walipitia taarifa hiyo na kuipitisha.

**MUHTASARI NA. 06/2021/2022:- KUPITIA TAARIFA YA MANUNUZI YA JENGO LA OFISI YA HALMASHAURI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021.**

Katibu wa Bodi aliwasilisha taarifa ya manunuzi ya vifaa kwa ajili ya jengo la ofisi ya Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na wajumbe kuipokea.

Akiwasilisha aliwaeleza wajumbe kuwa hadi Juni 2021 gharama za manunuzi ya vifaa vya ujenzi wa jengo la Halmashauri zimefikia shilingi 999,770,000 kati ya shilingi 1,000,000,000.00 zilizotolewa ikiwa ni manunuzi ya vifaa na malipo ya fundi.

Bodi ilipitia taarifa ya mchanganuo wa manunuzi ya vifaa kwa ajili ya jengo la ofisi ya Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2020/2021, ilijadili na kuipitisha kwa kushauri kiasi cha fedha kilichobaki 230,000.00 kifanyiwe manunuzi ya vifaa vya ujenzi kwa mujibu wa taratibu.

**MUHTASARI NA. 07/2021/2022:- KUPITIA TAARIFA YA MANUNUZI YA HOSPITALI YA WILAYA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021.**

Katibu wa Bodi aliwasilisha taarifa ya manunuzi ya vifaa na gharama za fundi kwenye ujenzi wa Hospitali ya Wilaya kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na wajumbe kuipokea.

Akiwasilisha aliwaeleza wajumbe kuwa hadi Juni 2021 gharama za manunuzi ya vifaa vya ujenzi wa jengo la Halmashauri zimefikia shilingi 577,961,120 kati ya shilingi 1,000,000,000.00 zilizotolewa ikiwa ni manunuzi ya vifaa na malipo ya fundi.

Wakati wa kupitia taarifa Bodi ilipitia michanganuo ya manunuzi ambapo walibaini kutokuwepo kwa taarifa za Islamic Help hivyo walitaka kufahamishwa taarifa za manunuzi ya ujenzi wa majengo ya Hospitali ya Wilaya yanayofadhiliwa na Islamic Help zitawasilishwa lini.

Akitoa ufafanuzi Katibu wa Bodi aliwafahamisha wajumbe kuwa fedha/kazi zitakazotekelezwa kwa ufadhili wa Islamic Help hazijumuishwi kwenye taarifa za Bodi ya Zabuni kwa sababu mradi huo utatekelezwa na kulipwa na mfadhili mwenyewe. Pia Mkataba wa makubaliano upo kati ya Serikali/Halmashauri ya Wilaya na Islamic Help hivyo Bodi ya Zabuni ~~haitambuliki.~~ haihusiki

Bodi ilipokea taarifa ya manunuzi ya vifaa na gharama za fundi kwenye ujenzi wa Hospitali ya Wilaya kwa mwaka wa fedha 2020/2021, ilijadili na kuipitisha.

**MUHTASARI NA. 08/2021/2022:- MAOMBI YA KIBALI CHA KUTEKELEZA MIRADI YA MAENDELEZO KWA NJIA YA NGUVU KAZI (FORCE ACCOUNT).**

Katibu wa Bodi aliwasilisha taarifa ya maombi ya kibali cha kutekeleza miradi ya maendelezo kwa njia ya nguvu kazi (Force Account) na wajumbe kuipokea.

Akiwasilisha aliwaeleza wajumbe kuwa miradi inayoombewa kibali cha kutekelezwa ni ile iliyotengewa fedha za bajeti ya mwaka 2021/2022 ambayo ni ujenzi wa jengo la

Utawala la Halmashauri, ujenzi wa Hospitali ya Wilaya, ujenzi wa nyumba za watumishi, ukamilishwaji wa ujenzi wa vyumba vya madarasa ya shule za msingi, umaliziaji wa ujenzi wa maabara za sekondari, ukamilishaji wa ujenzi wa zahanati, lipa kulingana na matokeo (EP4R) na miradi ya SEQUIP.

Wajumbe walijadili taarifa hiyo na kuridhia kwa ajili ya utekelezaji.

**MUHTASARI NA. 09/2021/2022:- MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI.**

**i. Bodi ya zabuni kujengewa uwezo kwa kupatiwa mafunzo**

Bodi ilijulishwa kuwa wajumbe wa Bodi wanaendelea kutekeleza majukumu yao lakini hawajapata mafunzo yoyote kuhusiana na sheria za uendeshaji wa bodi na taratibu za manunuzi. Alipendekeza Halmashauri ifanye taratibu za kuwezesha mafunzo wajumbe hao ili kujua majukumu na taratibu za uendeshaji wa Bodi.

Bodi ilijadili na kuridhia taratibu za mawasiliano na Afisa Masuuli zifanyike ili kufanikisha taratibu za mafunzo kwa wajumbe wa Bodi ya Zabuni kwa manufaa ya Halmashauri.

**ii. Vikao vya Bodi kufanyiwa malipo ya Posho za wajumbe kwa mujibu wa taratibu.**

Bodi ilijulishwa kuwa katika kipindi cha mwaka 2020/2021 Halmashauri ya Wilaya ilifanya vikao vyake vya bodi kwa mujibu wa taratibu ambapo vikao vya robo vilifanyika. Pamoja na Bodi kufanya vikao hivyo taratibu za malipo ya wajumbe wake hazikuweza kufanyika.

Bodi ilijadili na kukubaliana kuwa Sekretarieti ifanye taratibu za maandalizi ya maombi ya posho za vikao vya Bodi na nakala za maombi hayo ziwaslishwe kwa Afisa Masuuli kwa ajili ya hatua zaidi za maamuzi ya malipo hayo.

**MUHTASARI NA. 10/2021/2022:- KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti alifunga kikao saa 07.24 mchana.

**MUHTASARI UMETHIBITISHWA**

| **KATIBU** | **MWENYEKITI** |
|---|---|
| **JINA:** Bw. Brian John Munga | **JINA:** Bw. Napoleon Mlowe |
| **SAINI:** ..........(signed).......... | **SAINI:** ..........(signed).......... |

**TAREHE:** 28/08/2021

## YATOKANAYO NA MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA TAREHE 05/07/2021

| MUHT. NAMBA | AGIZO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| 04/2021/2022 | Bodi ya Zabuni ilipokea, ilijadili na kuipitisha taarifa ya manunuzi ya Halmashauri yaliyofanyika katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka wa fedha 2020/2021 na kuagiza yafuatayo:-<br>i. Taarifa ya mchanganuo wa manunuzi ioneshe aina ya kifaa kilichonunuliwa au huduma iliyotolea pamoja na gharama zake.<br>ii. Taarifa ya manunuzi yaliyofanyika katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2020/2021, Idara ya Elimu ~~msingi na~~ sekondari hazikuonekana na haikuwasilishwa hivyo Bodi iliagiza wakati wa kuandaa michanganuo ya taarifa za manunuzi ufuatiliaji wa karibu ufanyike na taarifa zioneshwe Ki-idara. Aidha taarifa ya manunuzi ya Idara za Idara za ~~Msingi na~~ Sekondari ziwasilishwe kikao kijacho. | Katibu wa Bodi ya Zabuni | |
| 09/2021/2022 | **Wajumbe wa Bodi ya zabuni kujengewa uwezo kwa kupatiwa mafunzo.**<br>Bodi ilijulishwa kuwa wajumbe wa Bodi wanaendelea kutekeleza majukumu yao lakini hawajapata mafunzo yoyote kuhusiana na sheria na taratibu za manunuzi kuhusiana na uendeshaji wa bodi. Ilipendekezwa Halmashauri ifanye taratibu za kuwezesha mafunzo kwa wajumbe hao ili kujua majukumu na taratibu za uendeshaji wa Bodi. | Katibu wa Bodi ya Zabuni | Barua ya kumwomba Afisa Masuuli kuwezesha Bodi elimu ya uendeshaji |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 09/2021/2022 | **Vikao vya Bodi [illegible]fanyiwa malipo ya Posho za wajumbe kwa mujibu wa taratibu.**<br>Kamati ilijulishwa kuwa katika kipindi cha mwaka 2020/2021 Halmashauri ya Wilaya ilifanya vikao vyake vya bodi kwa mujibu wa taratibu ambapo vikao vya robo vilifanyika. Pamoja na Bodi kufanya vikao hivyo taratibu za malipo ya wajumbe wake hazikuweza kufanyika.<br><br>Bodi ilijadili na kukubaliana kuwa Sekretarieti ifanye taratibu za maandalizi ya maombi ya posho za vikao vya Bodi na nakala za maombi hayo ziwaslishwe kwa Afisa Masuuli kwa ajili ya hatua zaidi za maamuzi ya malipo hayo. | Katibu [illegible] Bodi ya Zabuni | Madokezo ya kuomba Malipo ya Wajumbe wa Bodi yameandaliwa yapo kwenye taratibu za Malipo. |